# Maswali Yanayoulizwa Sana (FAQs) Kuhusu Pandemic EBT (P-EBT) ya Shule

*kwa Mwaka wa Masomo wa 2022-2023* *(Tarehe 4 Januari 2023)*

---

**Swali la 1: P-EBT ni nini?**

**Jibu**: Ni msaada wa chakula wa muda ulioidhinishwa na serikali ya shirikisho kusaidia familia ambazo zimeathiriwa na kufungwa kwa shule na mwanafunzi kutohudhuria shule kwa sababu ya COVID-19.

---

**Swali la 2: Ni nani anayestahiki kupata msaada wa P-EBT?**

**Swali:** Familia za Vermont zilizo na wanafunzi ambao kwa kawaida wangepokea milo ya bila malipo au iliyopunguzwa bei shuleni chini ya Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni (tafadhali pia angalia Swali la 3 kuhusu milo ya shule kwa wanafunzi wote katika mwaka huu wa shule). Msaada unapatikana kwa mwezi ikiwa:

- mwanafunzi amekosa kuhudhuria kwa udhuru kwa sababu ya COVID katika mwezi huo, **na**
- shule ya mwanafunzi huyo ilikuwa "inastahiki" kupokea msaada wa P-EBT. *Angalia mpango wa jimbo ili upate maelezo zaidi kuhusu jinsi shule hustahiki kupokea msaada wa P-EBT: https://dcf.vermont.gov/esd/P-EBT.*

---

**Swali la 3: Itakuwaje kwa wale wanaopata msaada wa milo kwa watu wote shuleni katika Vermont? Je, hii itaathiri kustahiki wa msaada wa P-EBT?**

**Jibu:** Bunge la Vermont lilipitisha sheria, Sheria ya 151 (2022), inayotoa ufadhili wa jimbo kwa milo kwa wote shuleni katika Vermont katika shule zote za umma na baadhi ya shule za kujitegemea. Hii inamaanisha kwamba kila shule ya umma na baadhi ya shule za kujitegemea katika Vermont zinashiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni na kustahiki mpango wa CEP au Provision 2 katika mwaka wa masomo wa 2022-2023. Mara tu kila shule inapostahiki (angalia Swali la 2 hapo juu), wanafunzi wote katika shule hii watakaokosa kuhudhuria shule kwa sababu inayohusiana na COVID watapata msaada wa P-EBT kwa siku walizokosa. Katika shule za kujitegemea zinazoshiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni na zinazotoza familia kwa chakula cha shuleni, wanafunzi wao watapata msaada iwapo tu wanastahiki kupata milo ya bila malipo au iliyopunguzwa bei.

---

**Swali la 4: Kutohudhuria kwa udhuru kwa sababu ya COVID kunamaanisha nini?**

**Jibu:** Kutohudhuria shule kwa sababu ya COVID kunamaanisha kutohudhuria shule wakati wa mwezi kutokana na mojawapo ya sababu zifuatazo:

- Uligunduliwa kuwa na COVID au ulikuwa na ugonjwa unaodhaniwa kuwa COVID,
- Ulitambuliwa kuwa ulikaribiana kwa karibu na mtu aliyeambukizwa COVID,
- Ulikuwa na dalili za COVID zinazosababisha haja ya kujiweka karantini na/au kupimwa COVID, au
- Shule, gredi au darasa lilifungwa au kuhamishwa kwa masomo ya mbali kwa ghafla kwa sababu inayohusiana na COVID, ikiwa ni pamoja na kisa cha maambukizi, uhaba wa wafanyakazi kwa sababu ya COVID, hitaji la kufuatilia watu waliokaribiana na mtu aliyeambukizwa, n.k.
- Kwa maelezo zaidi kuhusu kutohudhuria kwa sababu ya COVID-19, tafadhali angalia https://education.vermont.gov/documents/definition-of-covid19-related-absences-for-purposes-of-issuing-pebt-benefits

---

**Swali la 5: Shule yetu ilifungwa kutokana na matatizo ya theluji au kwa sababu ya kupasuka kwa bomba la maji au mfumo wa joto uliovunjika. Je, hizo ni sababu za kutosha za kuwastahiki wanafunzi kwa msaada wa P-EBT kwa siku hizo ambazo hawakusoma?**

**Jibu:** Hapana, sababu ya kufungwa kwa shule lazima ihusiane na COVID.

---

**Swali la 6. Je, nitajuaje kama familia yangu inastahiki msaada?**

**Jibu:** Shule ya mwanafunzi wako itabaini ikiwa mwanafunzi wako anastahiki, kulingana na vigezo vilivyotolewa na Jimbo la Vermont. Shule inaweza kuwasiliana nawe ili kuhakikisha kuwa ina taarifa sahihi kwenye rekodi zake. Tafadhali jibu ombi lao. Iwapo unastahiki, utapata barua kutoka kwa Idara ya Watoto na Familia (DCF, Department for Children and Families) inayoeleza jinsi na lini utapokea msaada.

---

**Swali la 7: Nilipokea kadi ya P-EBT mwaka uliopita wa shule (2021-22), lakini sina kadi hiyo tena. Je, hilo litakuwa tatizo?**

**Jibu:** DCF inaweza kukutumia kadi mpya. Maagizo yatajumuishwa katika barua za notisi ya msaada zitakazotumiwa katika mwezi wa Aprili 2023. Tafadhali tunza vizuri kadi yako mpya ukiipata. Huenda msaada wa ziada ukaongezwa kwenye kadi hiyo kwa kuwa kutakuwa na zaidi ya duru moja ya malipo katika mwaka huu wa masomo.

---

**Swali la 8: Msaada utatumwa lini?**

**Jibu:** Duru ya kwanza ya msaada kwa *Septemba 2022 hadi Januari 2023* itatumwa katika mwezi wa Aprili 2023. Msaada wa *Februari 2023 hadi Juni 2023* umepangwa kutumwa katika

mwezi wa Agosti 2023. Tafadhali endelea kuangalia Maswali Yanayoulizwa Sana kwenye tovuti ya DCF kwa taarifa mahususi zaidi: https://dcf.vermont.gov/esd/P-EBT. Tafadhali kumbuka kuwa serikali ya shirikisho itakomesha msaada wa P-EBT mwaka huu wa masomo ikiwa dharura ya shirikisho ya COVID-19 itaisha katika mwaka huu wa masomo. Ikiwa hali itakuwa hivyo, Maswali Yanayoulizwa Sana yatasasishwa ili kutambua mwezi wa mwisho ambapo msaada wa P-EBT utapatikana.

---

**Swali la 9: Msaada wa P-EBT ni kiasi gani?**
**Jibu:** Msaada wa P-EBT ni wa kiasi cha $8.18 kwa kila siku ambayo mwanafunzi alikosa kuhudhuria kwa udhuru kwa sababu ya COVID.

---

**Swali la 10: Je, msaada wa P-EBT ni wa kiasi sawa bila kujali idadi ya watoto katika familia?**
**Jibu:** Kiasi cha msaada wa kila mwezi ni mahususi kwa kila mwanafunzi kulingana na idadi ya siku alizokosa kuhudhuria kwa udhuru kwa sababu ya COVID katika kila mwezi. Familia zitapokea kiasi tofauti cha msaada kulingana na idadi ya siku kila mwezi ambazo kila mtoto katika familia alistahiki msaada wa P-EBT.

---

**Swali la 11: Malezi ya mwanafunzi wangu yamegawanywa kati ya familia mbili. Ni familia gani itapokea msaada?**
**Jibu:** Msaada utatumwa kwa mtu mzima aliyeorodheshwa kama "kiongozi wa familia" (head of household) katika rekodi za shule ya mwanafunzi. Huyu anaweza kuwa mtu mzima aliyetuma ombi la milo ya bila malipo na iliyopunguzwa bei kwa ajili ya mwanafunzi, au mtu mzima aliyeorodheshwa kama mwasiliani mkuu katika mfumo wa shule. Shule zinawasiliana na familia katika mwezi wa Januari ili kuthibitisha ni nani anayefaa kuorodheshwa kama "kiongozi wa familia". Tafadhali wasiliana na shule ikiwa "kiongozi wa familia" anahitaji kubadilishwa.

---

**Swali la 12: Ni bidhaa gani ninazoweza kununua na msaada huu?**
**Jibu:** Angalia bidhaa cha chakula unazoweza kununua ukitumia msaada wako wa P-EBT kwenye tovuti ya USDA: https://www.fns.usda.gov/snap/eligible-food-items.

---

**Swali la 13: Ni maduka gani ninayoweza kutumia kadi yangu ya P-EBT?**
**Jibu:** Unaweza kuitumia kununua vyakula vinavyoruhusiwa katika duka lolote linalokubali mpango wa 3SquaresVT. Hizi ni pamoja na maduka ya vyakula, maduka makubwa, maduka ya karibu na masoko mengi ya wakulima katika Vermont. Pata maelezo zaidi katika tovuti ya DCF katika https://dcf.vermont.gov/benefits/ebt.

---

**Swali la 14: Sina watoto wowote wanaoenda shule. Naweza kupata msaada huu?**

**Jibu:** Msaada huu ni kwa familia ambazo watoto wao kwa kawaida hupata milo ya bila malipo au iliyopunguzwa bei shuleni kupitia Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni na sasa wanahitaji kula vyakula hivyo nyumbani kwa sababu ya kutokuwepo kutokana na COVID na pia kwa wanafunzi wa masomo ya nyumbani wanaokidhi masharti yaliyoorodheshwa katika Swali la 16.

---

### Swali la 15: Je, msaada huu unalenga tu watoto katika shule za umma?

**Jibu:** Hapana. Baadhi ya shule za kujitegemea hushiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni, na watoto katika shule hizi wanaweza kustahiki msaada huu. Hata hivyo, shule nyingi za kujitegemea hazishiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni, na wanafunzi wao hawastahiki kupata msaada huu.

---

### Swali la 16: Mtoto wangu anafundishiwa nyumbani mwaka huu. Je, tunastahiki msaada huu?

**Jibu:** Unaweza kustahiki msaada wa P-EBT katika mwaka huu wa masomo kulingana na mwongozo mpya wa serikali ya shirikisho. Wanafunzi wafuatao wanaofundishiwa nyumbani wanaweza kustahiki msaada wa P-EBT mwaka huu:

- mwanafunzi ameandikishwa kupitia Shirika la Elimu (Agency of Education) kwa masomo ya nyumbani katika mwaka wa masomo wa 2022-2023
- mwanafunzi aliandikishwa katika masomo ya nyumbani wakati fulani baada ya tarehe 27 Januari 2020 (wanafunzi walioandikisha katika masomo ya nyumbani kabla ya tarehe 27 Januari 2020 hawastahiki)
- ikiwa mwanafunzi hajawahi kuhudhuria shule ya Vermont ana kwa ana, iwe kwa sababu yeye ni mgeni katika Vermont tangu Januari 2020 au mtoto huyo yuko katika shule ya chekechea, gredi ya kwanza au ya pili katika mwaka huu wa masomo, mzazi/mlezi anajaza uthibitisho unaosema kwamba mtoto anafundishiwa nyumbani katika mwaka huu wa masomo kwa sababu ya wasiwasi kuhusu COVID.

---

### Swali la 17: Je, familia zilizojiandikisha katika masomo ya nyumbani kupitia Shirika la Elimu zinahitaji kutuma ombi la msaada wa P-EBT ili kuupokea katika mwaka huu wa masomo?

**Jibu:** Hapana. AOE na DCF zitatumia maelezo ya uandikishaji wa masomo ya nyumbani kwenye rekodi zao ili kutoa msaada wa P-EBT wa masomo ya nyumbani. Kwa sababu shule zote za umma katika Vermont zinatoa chakula bila malipo kupitia Provision 2 na CEP, wanafunzi wote wa masomo ya nyumbani wanaotimiza masharti yaliyoorodheshwa katika Swali la 16 wataweza kupokea msaada bila kulazimika kuonyesha kwamba wanastahiki

milo ya bila malipo na iliyopunguzwa bei shuleni. AOE itawasiliana na familia za wanafunzi wa masomo ya nyumbani ikiwa kuna maswali yoyote kuhusu uandikishaji au maelezo ya mawasiliano kwenye rekodi za AOE na pia kujaza uthibitisho kwa familia zinazohitaji kuujaza ili kuthibitisha kwamba mtoto wao anasomea nyumbani mwaka huu kwa sababu ya wasiwasi unaohusiana na COVID.

---

**Swali la 18: Msaada wa P-EBT wa masomo ya nyumbani ni wa kiasi gani?**
**Jibu:** Msaada wa masomo ya nyumbani ni $143.15 kwa mwezi kwa kila mwezi kuanzia Septemba hadi Juni ambapo mwanafunzi ameandikishwa katika masomo ya nyumbani kupitia AOE. Tafadhali kumbuka kuwa serikali ya shirikisho itakomesha msaada wa P-EBT mwaka huu wa masomo ikiwa dharura ya shirikisho ya COVID-19 itaisha katika mwaka huu wa masomo. Ikiwa hali itakuwa hivyo, Maswali Yanayoulizwa Sana yatasasishwa ili kutambua mwezi wa mwisho ambapo msaada wa P-EBT utapatikana.

---

**Swali la 19: Je, msaada wa P-EBT wa masomo ya nyumbani utatolewa lini?**
**Jibu:** Msaada wa masomo ya nyumbani utatolewa kwa kwa pamoja katika mwezi wa Mei 2023 na utajumuisha msaada wa Septemba hadi Juni, isipokuwa dharura ya afya ya serikali ya shirikisho itaisha kabla ya Juni. Ikiwa hali itakuwa hivyo, Maswali haya Yanayoulizwa Sana yatasasishwa ili kutambua mwezi wa mwisho ambapo msaada wa P-EBT utapatikana kwa mwaka huu wa masomo.

---

**Swali la 20: Shule inapofungwa au mtoto wangu hajahudhuria, huwa tunaendea milo ya kwenda na kuchukua au shule hutuma milo nyumbani. Je, nitalazimika kuacha kufanya hivyo nikipata msaada wa P-EBT? Je, hiyo itafanya tusistahiki msaada?**
**Jibu:** Hapana. Wanafunzi wanaopokea milo kwa siku za masomo ya mbali bado wanastahiki msaada wa P-EBT. Bado unaweza kupata milo hiyo na ustahiki kupata msaada huu.

---

**Swali la 21: Nina watoto wengine ambao hawajaandikishwa shuleni au kwenye masomo ya nyumbani. Wanastahiki msaada huu?**
**Jibu:** Hapana. Msaada huu unapatikana tu kwa watoto ambao wameandikishwa katika shule ambayo kwa kawaida hushiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni au wanafunzi wanaostahiki walioandikishwa katika masomo ya nyumbani kupitia AOE ambao wanakidhi vigezo katika Swali la 16.

---

**Swali la 22: Watoto wangu wanahudhuria shule ya kujitegemea ambayo inashiriki katika Mpango wa Kitaifa wa Chakula cha Mchana cha Shuleni. Watoto wangu hawakustahiki kupata milo ya bila malipo au iliyopunguzwa bei hapo awali, lakini hali yetu sasa imebadilika. Naweza kupata msaada wa P-EBT?**

**Jibu:** Ikiwa hali yako ya kifedha imebadilika, tunakuhimiza utume ombi la msaada wa:

- **3SquaresVT** - ikiwa unapata msaada wa kila mwezi, mtoto wako anastahiki kupata milo ya bila malipo shuleni na anaweza kupokea msaada wa P-EBT. Jua jinsi ya kutuma ombi kwenye tovuti ya DCF katika https://dcf.vermont.gov/benefits/3SquaresVT.
- **Milo ya bila malipo au iliyopunguzwa bei** – pata fomu ya ombi kutoka shule ya mtoto wako au kwenye tovuti ya Shirika la Elimu: https://education.vermont.gov/. Maombi yaliyoidhinishwa yaliyotumwa kwa shule yako yanaweza kufanya familia yako istahiki msaada ya kuanzia Septemba 2022.

---

**Swali la 23: Itakuwaje ikiwa sitaki msaada huu?**

**Jibu:** Ni hiari kushiriki. Ikiwa utachagua kutoshiriki, basi:

- Usitumie msaada wa ziada unaowekwa kwenye kadi yako ya 3SquaresVT EBT. *AU*
- Tupa kadi yako binafsi uliyopewa ya P-EBT kwa kukata ukanda wa sumaku na kuitupa kadi hiyo kwa njia salama. HUPASWI kumpa mtu mwingine kadi yako.

---

**Swali la 24: Je, msaada wa P-EBT utaisha ikiwa hautatumika?**

**Jibu:** Ndiyo. Muda wa msaada wa P-EBT utakwisha ikiwa kadi haitatumika ndani ya siku 274.

---

**Swali la 25: Nina maswali zaidi. Ninaweza kupata wapi maelezo zaidi?**

**Jibu:** Nenda kwenye https://dcf.vermont.gov/esd/P-EBT au piga simu 1-800-479-6151, chaguo la 7, kwa maelezo zaidi. Tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi wako ikiwa una wasiwasi mahususi kuhusu kustahiki kwa mwanafunzi wako kwa milo ya bila malipo na iliyopunguzwa bei au ungependa kubadilisha kiongozi wa familia au anwani ya barua ambayo itatumika kutuma kadi.